

## Kuna Mfano

Katika Waebrania 9:18-23, twasoma ya kwamba Mungu alianziasha Agano la kale kwa damu... “Kwa hiyo hata lile la kale halikuanzwa pasipo damu... Hii ni damu ya agano mliloamuriwa na Mungu...Na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo,” 9:18,20,22. Kisha, katika mstari wa 23 twasoma, “Basi, ilikuwa sharti nakala za mambo ya mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo.” Hitimisho jepesi ambalo laweza kusababishwa na haya yote ni kuwa Mungu aliweka mfano. Pasipo msamaha wa dhambi na Agano haliwezi kuthibitishwa bila kumwagika damu, (Matendo 10:28; Mathayo 26:28)

Maelekezo! Nitakubali, mimi sipendi maelekezo/maagizo ambayo unaweza kuyakuta kwenye kifungashio cha bidhaa ambapo bidha inatakiwa ifungashwe. Huwa nayaangalia na kufikiri, huu ni uharibifu wa mti, na nayasweka kando. Halafu, ninapokuwa nimefungasha, naweza kuyaangalia maelekezo ili kuona kwanini nimebakiwa na vipande vingine (Lakini wote tunatambua kuwa si kosa langu!). Tuweke kando utani, sote tunajua kuwa kama tunataka bidha ifungashwe vyema, ni bora kufuata maelekezo. Tunapokuwa wabishi kufuata mfano, ndipo tunapojikuta kwenye matatizo.

Yesu alipokuwa katika sayari ya dunia, alijua kwanini alikuwepo duniani. Alijua analotakiwa kulifanya. Lakini ubinadamu aliokuwa nao ultamani namna nydingine. Lakini hakukuwa na nmna nydingine. Baba alitaka Yesu afuate mfano aliouweka. Yesu alitakiwa kumwaga damu yake. Kumwagika damu kwa ajili ya ondoleo na kulithibitisha agano ulikuwa ni mwongozo wa Mungu, na haukutakiwa kuswekwa kando, hata na mwanawе.

Sasa tuna utaratibu wa kufuata, Warumi 16:17; 1 Wakorintho 4:17; 2 Timotheo 1:13; Tito 2:7. Jambo ambalo litatupa kufikiria kwamba hatuwezi kumpendeza Mungu bila kufuata utaratibu ambao ameuweka ili tuufuate na kuutekeleza. Jambo ambalo linatufanya tuone kuwa sisi ni watu maalum kuliko Yesu. Ni wazi kuwa wengi walio katika ulimwengu wa dini leo na hata ndugu walio ndani ya Kanisa bado wanaamini kuwa wataokolewa na bila kuwa na utaratibu wa kuutekeleza ambao umewekwa katika Agano Jipy. Lakini endapo Yesu alitakiwa kuufuata utaratibu, ni nini kinachotufanya tudhani ya kuwa sisi ni bora kuliko yeye hata tusiufuate utaratibu? Tunaufuata utaratibu uliowekwa kwenye neno la Mungu? Neno la Mungu ndilo utaratibu ambalo kwalo unafuatisha

maisha yako, ibada na uongozi wa kanisa? Kama hapana, hivi hapo unakuwa unamaanisha nini?